# Je, kuna vipimo ambavyo vinaweza kugundua hali ya kuwepo kwa ualbino wakati kichanga kikiwa bado tumboni?

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Hakuna kipimo rahisi cha kuwezesha kuonyesha kama mama mjamzito amebeba kinasaba cha ualbino. Lakini uwezekano upo, kama wazazi watakuwa wamepata mtoto Albino. Uwezekano wa kujua kama mimba inayofuatia kichanga kitakuwa na ualbino kwa kutumia kipimo maalamu kinachovuta maji yaliyo kwenye mji wa mimba na kupima hayo majimaji kuona kama kuna kinasaba cha Albino. Hata hivyo, vipimo hivi ni vya gharama kubwa na kwa kiasi kikubwa kwa sasa vinapatikana, katika hospitali kubwa maalumu za nchi zilizoendelea (Ulaya, Marekani na kadhalika).